JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU

# Sera Bunge na Uratibu

JANUARI 2023

JARIDA LA MTANDAONI TOLEO LA KWANZA



KATIBU MKUU
OFISI YA WAZIRI MKUU SERA BUNGE NA URATIBU
2 BARABARA YA POSTA 40412 DODOMA TANZANIA

www.pmo.go.tz

# “Tatueni changamoto za Wananchi”
## Waziri, Simbachawene




Waziri wa Nchi Ofisi ya waziri Mkuu anayeshughulikia masuala ya Sera Bunge na Uratibu Mhe. George Simbachawene amewataka watendaji wa Serikali kuendelea kutatua changamoto za wananchi zinazowakabili ili kuchochea kasi ya maendeleo nchini.

Waziri ametoa kauli hiyo wakati akifungua mafunzo ya siku mbili ya kujenga uwezo kwa Menejimenti ya Ofisi ya Waziri Mkuu yaliyolenga kuwajengea uelewa kuhusu Idara ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Utendaji wa Shughuli za Serikalini yaliyofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Ofisi ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi uliopo Njedengwa Jijini Dodoma

Waziri alihimiza kila mtendaji wa Serikali kuhakikisha anatekeleza majukumu yake kwa ufanisi huku akitatua changamoto za wananchi katika eneo lake la kazi.

Aliongezea kuwa ni muhimu kwa watendaji kuwajibika kwa kuyafikia malengo ya Serikali ya Awamu ya Sita huku wakileta matokeo chanya yatokanayo na utendaji mzuri wa kazi zao za umma.

"Hakikisheni mnakuwa watu wa msaada kwa wengine katika kuyatekeleza majukumu yenu, muwe watengeneza furaha na hii iwe kipimo kwa kila mwenye kukufikia huku ukizingatia taratibu za utumishi wa umma na sheria zilizopo,"alisema Waziri Simbachawene

Aidha aliwaasa waendelee kutumia taaluma zao kuleta matokeo chanya kwa Serikali na jamii huku wakijitathimini utendaji wa kila siku

“Ni sahihi kujitathimini kila iitwapo leo ili kuona namna unavyoleta matokeo chanya kwenye utendaji wako wa kila siku, matokeo utayoyapata yatatusaidia kuongeza tija ,” alisisitiza Waziri Simbachawene.

Akieleza umuhimu wa mafunzo hayo aliwataka kuhakikisha mafunzo yanawafikia watendaji katika ngazi zote ili kuendelea kuongeza uelewa kwa watumishi wa umma.

"Hakikisheni mnakuwa watu wa msaada kwa wengine katika kuyatekeleza majukumu yenu, muwe watengeneza furaha na hii iwe kipimo kwa kila mwenye kukufikia huku ukizingatia taratibu za utumishi wa umma na sheria zilizopo,"alisema Waziri Simbachawene

Aidha aliwaasa waendelee kutumia taaluma zao kuleta matokeo chanya kwa Serikali na jamii huku wakijitathimini utendaji wa kila siku.

"Ni sahihi kujitathimini kila iitwapo leo ili kuona namna unavyoleta matokeo chanya kwenye utendaji wako wa kila siku, matokeo utayoyapata yatatusaidia kuongeza tija ," alisisitiza Waziri Simbachawene.

Akieleza umuhimu wa mafunzo hayo aliwataka kuhakikisha mafunzo yanawafikia watendaji katika ngazi zote ili kuendelea kuongeza uelewa kwa watumishi wa umma.


" Mafunzo haya yawafikie watumishi wote katika Idara na vitengo vyetu bila kumuacha nyuma mtu yeyote ili kuleta chachu katika utendaji na kuondokana na tabia ya mazoea," alisema.

Aliongezea kuwa matokeo ya Mafunzo haya yatumike kuboresha mifumo ya uratibu, usimamizi na ufuatiliaji wa shughuli za Serikali ili kuwa na uwezo wa kupima utendaji wa Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali kisayansi.

"Ili kuendelea kuboresha shughuli za uratibu naamini uwepo Idara mpya ya Ufuatiliaji na Tathmini itasimamia hili na kuhakikisha kunakuwa na mrejesho kwa Wizara na Taasisi zote ili kuimarisha uwajibikaji," alihimiza.

Kwa upande wake Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu Dkt. John Jingu amesema mafunzo haya yanalenga watendaji wa serikali kufanya kazi kwa ufanisi kwa weledi na kwa namna ambayo itakidhi mahitaji pia yatajikita katika majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu katika eneo la uratibu wa shughuli za serikali, na jukumu la kufanya kazi ya ufuatiliaji na tathmini ya utendaji wa shughuli za Serikali.

# Habari katika picha



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulika na Sera Bunge na Uratibu Mhe. George Simbachawene amewapongeza wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Sheria Ndogo kwa kazi kubwa ya kuchambua sheria Ndogo zilizowasilishwa katika mkutano wa tisa wa Bunge.

Waziri ameyasema hayo katika ukumbi wa Bunge Mjini Dodoma, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo inaisaidia Serikali ili iwezee kufanya mambo kwa kuzingatia haki na sheria.



# Serikali yatoa msaada kwa Waathirika wa Mafuriko ya maji Mkoani Mbeya

Serikali Kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu Sera Bunge na Uratibu imetoa msaada kwa wananchi walioathirika na Maafa ya Mafuriko ya Maji Mkoani Mbeya, yaliyosabisha nyumba kubomoka, kuharibika kwa vifaa, vyakula, uharibifu wa mifugo na mazao yaliyoko mashambani.

"Msaada huo unajumuisha Magodoro 300 kwa kuanzia, mablanketi 1200 ya wakubwa na wadogo, mikeka 600, madumu ya maji, sufuria bakuli sahani pamoja na vijiko kwa kila familia ambayo imeathirika."

Kauli hiyo imetolewa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera Bunge na Uratibu Mhe. George Simbachawene alipotembelea maeneo yaliyoathirika wa mafuriko ya mvua katika kata saba Mkoani Mbeya kutokana na Mvua zilizonyesha

"Kwa mujibu wa sheria no. 6 ya Maafa ya Mwaka 2022 sisi kama Ofisi ya Waziri Mkuu tunayo dhamana ya kuwaunganisha wadau ili kuwasaidia watu walioathirika na tutafanya hivyo kwa kutumia Ofisi zetu za Mkoa na wilaya, naomba wadau wote wa ndani na nje ya Mkoa wa Mbeya kutusaidia ili kuhakikisha watu hawa wanarudi katika hali yao."

Natoa pole kwa wote walioathirika, TARURA kwa kushirikiana TANROAD Halmashauri ya jiji la Mbeya na Halmashauri ya Mbeya vijijini wahakikishe wanaenda kuona kwenye vyanzo kuangalia ni eneo gani maji yametoka kwenye mkondo wake wa asili.

Akimkaribisha Waziri wa Nchi, Mbunge wa jimbo la Mbeya Mjini na Spika wa Bunge la jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Tulia Ackson ameishukuru serikali kwa mchango iliyoutoa kwa waathirika wa mafuriko ya Mvua Mkoani Mbeya .

"Naomba sisi kama Halmashauri tusitoe vibali vya ujenzi kwenye maeneo ambayo ni mikondo ya maji, kwa sababu athari za mafuriko zinarudisha nyuma maendeleo ya uchumi kwa wananchi"

Naye Mkuu wa Mkoa wa Mbeya Mhe. Juma Homera katika taarifa yake amesema watu waliopata athari za mafuriko ya maji, kaya 281 zenye watu idadi ya watu 1405 ambao wanahitaji chakula takribani tani 50 kwa miezi mitatu ili ziweze kuwasaidia.

.

Waziri Simbachawene,

## aridhishwa na hatua ya ujenzi kiwanda kipya cha Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera Bunge na Uratibu ameridhishwa na kasi ya ujenzi wa kiwanda cha kupiga chapa cha serikali ambacho mpaka sasa msingi wa jengo na ujenzi wa boma la jengo; kuta, kupiga plasta na kupauwa vimeshafanyika.

"Hiki kiwanda tunatarajia kukifunga mitambo na mashine za kisasa ili kiweze kufanya jukumu la kuchapa nyaraka za Serikali na shughuli za Mpiga Chapa ziweze kufanyika kwa ufanisi."

Kauli hiyo ameitoa alipotembelea na kujionea maendeleo ya ujenzi wa kiwanda hicho cha Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kilichopo Kisasa katika Jiji la Dodoma .

Ofisi hii ni muhimu sana kwa nchi, ni lazima iwe Ofisi bora kwa sababu nyaraka nyingi za siri za serikali zinapaswa kuchapwa na Ofisi ya Mpiga Chapa wa Serikali.

Waziri Simbachawene amempongeza Rais Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda hicho cha mpiga chapa wa serikali kwa kiasi cha bilioni 1.8.

"Serikali imetoa pia kiasi cha million kiasi cha millioni 350 ambazo zitatumika kufanyia ukarabati kiwanda na Mashine za Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali Jijini Dar es Salaam ikiwa ni pamoja na kiasi kingine cha shilingi billioni 1.4 kwa ajili ya kununua malighafi kwa viwanda vinavyondelea na uzalishaji, cha Dodoma na Dar es salaam."

Amefafanua kiwanda kipya cha Dodoma cha Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali imetoa kiasi cha shilingi billioni 3.9 ambayo itasaidia kununua mitambo mipya na ya kisasa ili kuhakikisha nyaraka zote muhimu za serikali zinachapishwa katika kiwanda hicho.

"Nembo ya Taifa, Bendera ya Taifa na Mhuri ni vitu ambavyo vimewekwa katika uangalizi wa Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali."

Naye Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali Bwn. George Lugome ameishukuru Serikali ya Awamu ya Sita kwa kutoa fedha kwa ajili ya kuboresha idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kuiwekea majengo yenye uwezo wa kuwa na miundo mbinu mizuri na mashine za kisasa ambazo zitasaidia kuchapa nyaraka zenye alama ya siri.

“Sheria ya alama za Taifa ya mwaka 1971 inatamka wazi kabisa kwa yoyote anayekiuka au anaibadili nembo ya Taifa au alama za Taifa anastahili kupewa adhabu ya kifungo cha miaka miwili jela,” amesema Bwn, Lugome.

Ametoa wito kwa taasisi binafsi zinazotaka kujihusisha na uchapaji wa nyaraka kuhakikisha wanathibitishwa na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Usalama ya Serikali ili waweze kupata kibali.



# Dkt.Jingu: Matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi yatumike katika mipango ya maendeleo



Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia masuala ya Sera, Bunge na Utatibu Dkt. John Jingu ameeleza ni muhimu kuyatumia matokeo ya sensa ya watu na maakazi ya mwaka 2022 katika mipango mbalimbali ya maendeleo ya nchi yetu.

Ameyasema hayo wakati akiongoza kikao cha 9 cha Kamati ya Ushauri ya Taifa ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 kwa ajili ya kupitia baadhi ya ripoti za matokeo ya Sensa zilizo kamilika kabla ya kuzinduliwa.Kikao kilifanyika katika ukumbi wa Mikutano wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere Dar es Salaam.

Jukumu kubwa la Kamati hiyo ni kuishauri Kamati Kuu ya Taifa ya Sensa inayoongozwa na Mhe. Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar namna bora ya utekelezaji wa masuala ya sensa.

# Watumishi Ofisi ya Waziri Mkuu watakiwa kufanya kazi kwa ushirikiano.



Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulika masuala ya Sera Bunge na Uratibu Dkt. John Jingu, amewataka watumishi wa Ofisi hiyo kufanya kazi kwa ushirikiano ili kuwa na utendaji wenye matokeo.

Dkt. Jingu ameyasema hayo wakati wa mkutano wa watumishi wa ofisi yake uliofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Ofisi ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi uliopo Njedengwa Jijini Dodoma ambapo ulilenga kuwajengea uelewa kuhusu mada masuala ya Afya ya akili, magonjwa sugu yasiyoambukizwa na ulaji usiofaa pamoja na maadili mahali pa kazi.

Katibu Mkuu aliwasisitiza watumishi kutekeleza majukumu yao kwa weledi na ufanisi kwa kushirikiana ili kuyafikia malengo ya serikali kwa ujumla na kujiletea maendeleo.

Alisema kuwa ipo haja ya kuwa na mafunzo kwa kila mtumishi kwa kada zote ili kuwajengea uwezo utakaoleta tija katika kutekeleza majukumu yao.

"Inatubidi tufanye mafunzo ya muda mfupi katika vitengo na idara ili watu wapate ujuzi na hili ni jambo la muhimu katika kutusaidia kuongeza ufanisi na tija katika kazi," alisema Dkt. Jingu.

Alifafanua kuwa, vikao vya idara na vitengo kila wiki vitasaidia kuwa na uelewa wa pamoja juu ya majukumu tuliyonayo ambayo yatasaidia kuongeza ushirikiano na uwezo katika utendaji kazi wa kila siku.

"Lazima twende pamoja ili tufanye kazi kama timu, ili kuweza kufikia malengo, ambapo kuna malengo ya mtu binafsi na kuna malengo ya kiofisi, ustawi wa mtu mmoja ni muhimu katika kufanikisha malengo ya Ofisi na Serikali kwa ujumla". Alisisitiza.

.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa TUGHE, Tawi la Ofisi ya Waziri Mkuu Bi, Numpe Mwambenja ameishukuru ofisi kwa kuandaa mkutano huu wenye tija huku akisisitiza watumishi kuendelea kutekeleza majukumu kwa ushirikiano ili kuweza kutimiza malengo.

"Muongozo wa ugawaji wa majukumu ya utendaji kazi utasaidia kuongeza bidiii zaidi katika utendaji wa kazi wa kila siku na kutusaidia kupima utendaji wetu,"alisema Numpe

.

---

Jarida hili la Mtandao Limeandaliwa na kutolewa na
Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Ofisi ya Waziri Mkuu Sera Bunge na Uratibu



KATIBU MKUU
OFISI YA WAZIRI MKUU
2 MTAA WA RELINI, S.L.P 980
40480 DODOMA.
Barua pepe,ps@pmo.go.tz, Simu, +255262322480
Fax:+255262324534, Tovuti: www.pmo.go.tz